

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

Telegrams: "SIASA"
Telephone: 2137232
Fax: 2136924
(Unapojibu tafadhali taja)



Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Kivukoni Ilala CBD
1 Mtaa wa Shabani Robert
S.L.P. 63010
11101 – DAR ES SALAAM.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU WITO KWA VYAMA VYA
SIASA KUTII SHERIA WAKATI WA UCHAGUZI.**

Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Mhe. Jaji Francis S.K. Mutungi amevikumbusha vyama vya siasa kutii Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Gharama za uchaguzi na kanuni zake wakati wa uchaguzi.

Wito huo umetolewa kupitia barua aliyoviandikia vyama vya siasa yenye kumbukumbu HA.322/362/01/165 ya tarehe 30 Januari, 2018.

"...natambua kuwa baadhi ya vyama vyenu vinashiriki katika chaguzi ndogo za Ubunge na Udiwani zinazoendelea katika majimbo na kata. Hivyo, natumia fursa hii pia kuvipongeza vyama vyote vinavyoshiriki katika chaguzi hizo, kwa kushiriki katika tukio hili muhimu la kidemokrasia. Aidha, naviasa vyama vinavyoshiriki uchaguzi kuheshimu na kufuata sheria za nchi, hasa Sheria ya Vyama vya Siasa, Sheria ya Gharama za Uchaguzi na kanuni zake, kwa kuepuka vitendo vya fujo na lugha za matusi na uchochezi" imenukuliwa barua hiyo.

Jaji Mutungi pia ametoa wito kwa mwanachama wa chama chochote cha siasa au chama kinachoshiriki uchaguzi kutoa taarifa katika mamlaka husika kuliko kujichukulia sheria mkononi, endapo kitashuhudia kwa kuona ama kusikia uvunjifu wa Sheria unaohusu chaguzi zinazofanyika.

Imetolewa na;

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Monica Laurent'.

Monica Laurent
Mkuu wa kitengo cha Mawasiliano Serikalini
OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA.
31 Januari, 2018